102/3

KISWAHILI

KARATASI YA 3

FASIHI

MTIHANI WA KIDATO CHA 4

JULAI/AGOSTI 2018

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

**KIDAGAA KIMEMWOZEA**

1.(a) Maneno ya mtemi Nasaba bora akimwambia Amani.
Wakiwa kwa Mtemi baada ya Amani kumkabili na kumshurutisha amweleze ukweli kuhusu kuuliwa kwa babuye Chichiri Hamadi na kufungwa Yusufu. (4x1= 4)

(b) Chuku- wema wako umeniua kabisa
Jazaada – Kuna mahakama ndani moyo wangu.
Nahau - Miaka na mikaka
Tashihishi – wema kupewa uwezo wa kuua. (2x2=4)

(c) (i) Kumuua babuye . Amani
(ii) Kukataa kumsaidia/kumbeba mama aliyekuwa akijifunga kando ya barabara baada ya sherehe ya sikukukuu ya wazalendo.
(iii) Kumlazimisha Amani kukilea kitoto ‘uhuru’
(iv) Kumpiga Amani nusura amuue.
(v) Kumfanya Yusufu kufungwa jela kwa visingizio.
(vi) Kuwafanya Amani na Imani kuwekwa korokoroni kwa makosa ambayo alijua si yao.
(vii) Kuamrisha watu wasikubaliwe kuingia katika hema mvua uliponyesha wakati wa sherehe.
(viii) Kumpiga na kumpa talaka mkewe
(ix) Kumuua Paka kiunyama.
(x) Kutompeleka hospitali DJ anapong’atwa na mbwa.
(xi) Kuachilia mbwa wake kurandaranda akiwa mgonjwa.
(xii) Kutomsaidia Matuko Weye baada ya kutoka vitani.
(x) Kumtunga mimba msichana Lowela.

(ix) Kutupa mtoto mlangoni pa Amani.

(x) Kuacha mtoto katika baridi.

(xi) Kuacha mkewe katika upweke.

(xii) Kuwatupia watu chche za matugi.

(Zozote 12x1 = 12)

2.(a) Maneno ya Kenga akimwambia Majoka wakiwa ofisini mwa Majoka.

Wanazunguza kuhusu umaarufu wa Tunu uliokuwa ukizidi kuongezeka. (4 x 1= 4)

(b) Methali – Jambo linalokaribia kutendeka huonyesha daili kabla halijaendeka.

- Kenga anamtahadharisha Majoka kuwa kuna ishara tosha kuwa umaarufu wa tunu umeanza kuenea (1 x 2 = 2)

(c ) Kenga anamshauri Majoka atangaze kuwa maandamano ni haramu kisha aamuru polisi

watumie nguvu zaidi.

- Ana maana kuwa watu wengi wauliwe kuliko walivyowahi kuuliwa tangu mwanzo wa maandamano.

- Inaonesha hana huruma kwa Wanasagamoyo waliokosa ajira kwa kufungiwa soko. (2x2=4)

d) i) Unafiki ni hali ya mtu kujifanya kuwa bora au kujifanya kusema ukweli ilihali yu vingineyo.

- Kenga anajifanya kumshauri majoka lakini anampotosha kwa kauli zake kinzani.

- Anasema kuwa Tunu wadhibitishe ilhali mbeleni alikuwa amesema Tunu hana umaarufu na hawezi kupigiwa kura.

- Upumbavu ni hali ya mtu kutotambua mambo hata yale yaliyo dhahiri.

- Majoka anashindwa kungamua kwamba Kenga anampa ushairi wa uongo.

- Hawezi kungamua kwamba Kenga anajua ukweli na anampumbaza tu.

- Hakujua habari kuhusu idadi ya watu walio tayari kumpigia Tunu kura. (3x2=6)

(e) Kauli inadokeza kuwa umaarufu wa Tunu na watu wa mrengo wake unazidi kushamiri.

- Kampeni zake za kuwaazidwa Wanasagamoyo zinaelekea kufua dafu.
- Anafanikiwa kuwashawishi Wanasagamoyo kutohudhuria mkutano wa Majoka.
- Waliokuwa katika mrengo wa Majoka kama Mamapima, Kenga na Kingi wanamtoroka na kujiunga na Tunu. (2x2=4)

3.(i) Mgogoro kati wa wanandoa Ashua na Sudi.
Mgogoro huu ulichochewa na hali ngumu ya maisha ambapo Ashua anapotiwa kizuizini anasema amechoka kumuona Sudi akifuatana na Tunu. Pia anamlaumu mumewe kwa kushindwa kuikimu familia yake.
Suluhisho: Sudi anamshawishi mkewe asisikize umbea wa watu kama Majoka.

(ii) Mgogoro kati ya Viongozi na wanaharakati.
Unachochewa na uongozi mbaya wa Majoka. Majoka anafunga soko la chapakazi na Tunu anaongoza watu kuandamana ili lifunguliwe.
Suluhisho: Wanasagamoyo wanamwondoa Majoka mamlakani.

(iii) Mgogoro baina ya mafundi wa kuchonga vinyago.
Sudi na Boza wanagombana kwa sababu ya mitazamo yao. Boza ametosheka na uongozi wa Majoka ilihali Sudi anaupinga.
Suluhisho: Sudi anawasihi waungane naye na hatimaye kombe anazinduka.

(iv) Mgogoro wa nafsi

Babu anaichochea nafasi ya Majoka kuwa abadilishe mawazo na mienendo yake kwani wema hauozi.

Suluhisho: Majoka anakataa kuzinduka na hivyo haukusuluhishwa.

(v) Mgogoro baina ya vyombo vya habari na utawala.

Hii ni kutokana na hatua mbalimbali zinazohusu udhalimu wa serikali. Runinga ya mzalendo inapigwa marufuku baada ya kupeperusha habari kuhusu umaarufu wa Tunu.

Suluhisho: Watu wanauangusha utawala mbaya wa Majoka.

(vi) Mgogoro baina ya Majoka na Sudi.
Unatokana na kuwa wote wawili walimpenda Ashua. Majoka anataka Ashua amwache Sudi ili amwoe.

Suluhisho: Sudi anamhakikisha Ashua kuwa annemtunza na kumwomba asitititilie maanani umbeya wa Majoka.

(vii) Mgogoro baina ya nguruno na Sudi.
Ngurumo anamtuhumu Sudi kwa kusema kuwa alilala na Tunu.

Suluhisho: Sudi hakumhjali bali aliendelea na harakati na Tunu aliendelea na za kuwazindua wanajamii.

(viii) Mgogoro kati ya Kenga na Majoka. Kenga anakengeuka na kukubaliana na waandamanaji.

Suluhisho: Kenga anaungana na waandamaji na hatimaye kuangusha utawala wa Majoka.

(ix) Mgogoro kati ya Majoka na Kingi.
Kingi anakataa kutii agizo la kuwapiga risasi wananchi waliokusanyika katika soko la Chapakazi.

Suluhisho: Wanaouangusha utawala mbaya wa Majoka.

(ix) Mgogoro baina ya Tunu na Ngurumo.
Ngurumo anamdunisha. Tunu huku akisema kuwa hawezi kupatia/kupiga kura yake kwake. Hata anamwimbia wimbo.
Suluhisho : Tunu na Sudi wanamwacha ngurumo mangweni.

(ix) Mgogoro kati ya Husda na Ashua.
Husda anamchukia na kumpiga Ashua kwa kumtaka mumewe.
Suluhisho: Ashua anatiwa korokoroni.

(xii) Majoka na wananchi.

Wananchi wanajitokeza kuandmana ili kupinga uongozi mbaya wa Majoka. Majoka anamwamuru Kingi awapige risasi lakini alikataa.

Suluhisho: Wananchi wanauangusha utawala wa Majoka.

(Hoja zozote 10x2 = 20)

4.(a) Maneno yalisemwa na mwenye tumbo lisiloshiba
Anamwambia mzee Mago.
Wako kwenye hoteli ya mzee Mago.
Alikuwa amemaliza kula na alikuwa akidokeza kuwa keshoye angefika pale.

(4x1=4)

(b) Takriri – Kama … kama
Mdokezo . salama …..
Kisengere mbele/ mbinu elekezi
Kama tutafungua milango ya nyumba zetu.

(2x2=4)

(c ) Mlafi – anakula chakula chote kwenye mkahawa.
Mwenye tamaa – anatamani ardhi ya madongoporomoka.
Mdunishaji – Maslahi ya wengine hawajali wanamadongoporomoka watahamia wapi.
Mwenye upeo mfupi – Hakufikiria kuwa wanamadongoporomoka wangeweza kupingana naye na kukatia hapo.

Mwenye dharau – Anamtamkia mzee Mago kwa ujeuri na kusema 'Nimekuahidi kuja kula ardhi yako hii leo'.

Mkakamavu- hakujali kama watu wangemvamia alipokuwa akila chakula chote kwa mabavu huko kwa mzee Mago.

(6x1=6)

(d) (i) Ufisadi – Matajiri wamenyakua mali ya umma.

(ii) Unyakuzi wa ardhi – mwenye tumbo lisiloshiba anataka kunyakua mashamba ya Wanamadongoporomoka.

(iii) Nyakanyaka za nyumba – Nyumba nyingi sana zimejengwa kila mahali jijini.
(iv) Matumizi mabaya ya vyombo vya dola – askari wanatumiwa kawalinda mabwanyenye wanaonyakua ardhi.
(v) Ubomoaji wa vibanda – vibanda vya kina yahe vinabomolewa huko madongoporomoka.

(vi) Utabaka - Kuna matajiri na maskini. Matajiri wanaishi jijini nao maskini wanaishi madongoporomoka.
(vii) Maandamano – maskini wanahitajitetea kwa kuandaa maandamano.

6x1=6)

5. Ukengeushi ni hali ya kuacha njia nyofu na kufuata njia potovu.

- ✓ Viongozi wa kisiasa wamekengeuka kuwa kuwaua vijana ambao ni nguvi ya taifa.
- ✓ Vijana wamepotoka Kimaadili- Mkubwa aliona vijana wanalaliana nje hdharani, walipotambua wameonekana walikuwa tayari kuua watu kwa kisu au bisibisi.
- ✓ Vijana wamegeuka kuwa wezi na wanyanganyi watu mali zao.
- ✓ Vingozi wa serikali wanafanya biashara ya 'unga'bila kujali athari kwa vijana na taifa.
- ✓ Viongozi wanajitajirisha kuwa kuuza unga, wanaingiza bidhaa hii bandarini bila kukaguliwa.
- ✓ Unga unasababisha vijana wengi kuwa wanyonge na wasio na akili timamu. K.m mkubwa anamkuta kijana aliyetoa denda mdomoni.
- ✓ Vijana ni wapyoro – wanatumia lugha chafu ajabu.
- ✓ Tamaa ya utajiri inamfanya mkubwa kuingilia biashara ya kuuza dawa za kulevya.
- ✓ Mkubwa anauza shamba lake la urithi na kupata milioni kumi ambazo anatumia kuhonga wapiga kura.
- ✓ Mkubwa anatoa rushwa kuwa kiongozi wa askari waliokamata mzigo wake na pia mkumbukwa aachiliwe.
- ✓ Kuna ukosefu wa haki kuwa mahabusu waliowekwa kizuizini – wengi wao wanateswa kabla ya kuthibitishwa kuwa wahalifu.
- ✓ Viongozi wanatelekeza raia wengi kwa ukimwi na dawa za kulevya ambazo zinawadhuru.
- ✓ Wakubwa wanafungua majumba makubwa ya kurekebisha tabia, ilhali wao wangetakiwa warekebishwe tabia zao kwanza.
- ✓ Askari polisi hawafanyi kazi zao vizuri wanaruhusu 'vigogo' kupitisha dawa za kulevya nchini. n.k.

(Hoja zozote 10x2 = 20)

6. a)

- **Maudhui** ambayo huangaziwa katika fasihi simuklizi hujitokeza katika andishi. Hivyo basi fasihi andishi hujenga maudhui yake kutoka kwa yule ya fasihi simulizi.

- Tanzu za fasihi simulizi huwa na **dhamira,** mahususi kwa jamii kwa mfano kuadilisha. Vivyo hivyo fasihi andishi huwa na dhamira sawia na ilivyo kwa fasihi simulizi.

- Wingi wa tanzu za fasihi simulizi huambatana na **utendaji** zinapowalisishwa. Kipengele hiki pia kipo kwa tanzu za fasihi andishi kama vile tamthilia ambayo huigizwa.

- Fasahi simulizi na andishi pia hutumia nyenzo ya **lugha** kwa uwasihishaji. **Lugha** ndiyo nyenzo kuu itumiwayo kiufundi kama malighafi ya kubuni kazi ya kifasihi.

- Uwasilishsaji na fasihi simulizi una msingi wake kwa **usimulizi** ambao hutumiwa kueleza na kuwasilisha visa. Fasihi aindishi pia huwasilisha ujumbe wake kwa matumizi ya usimulizi.

- **Fani** zilizomo katika tanzu za fasihi simulizi kama vile ploti, na wahusika pia hubainika katika tanzu za fasihi andishi. (zozote 5x2 = alama 10; kutajaal.1, kueleza al.1)

(b)

- Huwasilisha kwa njia yam domo mbele ya hadhira kwa **kukaririwa** au kuimbwa.
- Hutumia lugha yenye **mvuto** na mapigo yanayopangwa kwa muwala na urari.
- Huweza **kuwasilishwa** na mtu mmoja kwa mfano majigambo au kundi la watu kwa mfano nyimbo.
- Huweza **kubuniwa** papo hapo na kuwasilishwa kwa hadhira au kutokana na kumbukumbu ya awali kuhusu vipera husika.
- Baadhi ya tungo zake huwasilishwa kwa kuambatana na **ala** za muziki kwa mfano uimbaji wa nyimbo.
- Huwa sehemu ya **utamanduni** wa jamii na maudhui yake hutegemea utamaduni huo ambao umerithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.
- Huweza **kubadilika** kulingana na anayewasilisha, hadhira legwa au wakati.
- Ushairi simulizi hutumia lugha ya **kitamathali** iliyojaa misemo, nahau, methali, jazanda n.k. ili kupamba uwasilishaji.
- Uwasilishaji wa mashairi simulizi humbatana na **uigizaji** / utendaji ambapo mwimbaji kwa mfano huambatanisha wimbo wake na vitendo au ishara mwafaka.
- Huweza kuwa na hadhara hai kutegema kipera. Kwa mfano mwimbaji wa wimbo anaweza kushirikisha **hadhira** kwa kupiga makofi au kuitika.
- Ushairi simulizi hufungamana na **muktadha** au shughuli maalum za kijamii. Kwa mfano wawe hufungamana na shughuli za kilimo.
- Huweza kuwa na **urari** wa vina na mizani au la, maadam kilicho muhimu ni mapigo ya kimziki.

(zozote 5x2= alama 10, kutaja alama 1, kueleza alama 1)

**7. Jibu la swali la shairi**

(a) Ni mashairi huru / Vue (1x1 = 1)

(b)(i) Mshairi A

\- Anamlalamikia Hadija kwa kumuua mumewe kwa kumpa sumu

(ii) Mshairi B

\- Anawalalamikia vijana ambao wanamcheka ati amezeeka na kupitwa na wakati. (wanamlamba kisogo) (2x2=4)

**(c ) Kinaya**

(i) Katika Shairi "A"

Hadija alidhani kumuua mume angepata suluhisho lakini badala yake amejiletea matatizo zaidi watu wanamsuta na watoto wanamsumbua.

(ii) Amemuua mumewe-mti mkuu au kichwa cha nyumba na sasa anapata shida za kujitakia (2x2=4)

(iii) Katika Shairi B

Vijana wanamsengenya na kumdhihaki mzee kwa uzee wake ilhali wao wanaendelea kuzeeka. Mzee anapowapisha, hawataki kupita. (1x2=2)

d) (i) Mzigo – uzee/umri

(ii) Siri- tajriba/maarifa/elimu ya maisha

(iii) Niko nyuma ya wakati – Nimebaki nyuma na usasa. 3x1=3

(e) **Lugha nathari**

Mzee anawataka vijana wapite na kwenda watakako kwani yeye hana haraka kwa sababu ana mzigo ambao hataki kuuweka chini. (alama 4)

(f) **Uhuru wa mashairi 'B'**

(i) Inkisari – nendako – niendako (alama 2)